# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## Uchambuzi wa Hotuba ya Rais Magufuli baada ya kufanya Mabadiliko madogo katika Baraza la Mawaziri

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimefuatilia kwa umakini hotuba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli aliyoitoa Jumatatu Julai 2, 2018 wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali walioteuliwa kuchukua nyadhifa mbalimbali Serikalini. Kupitia hotuba hiyo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini masuala chanya ambayo Kituo kimekuwa kikiyafanyia utetezi, lakini pia baadhi ya mambo hasi ambayo si shamirishi kwa haki za binadamu na utawala bora. Mbali na ukweli kwamba uteuzi huo haukuzingatia kabisa uwiano wa kijinsia, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeainisha masuala kadhaa ya kuungwa mkono kutoka katika hotuba ya Mhe. Dkt. Magufuli kama ifuatavyo:

1. Uwajibikaji wa watendaji na mamlaka za Serikali; Kupitia hotuba yake Rais Magufuli ameendelea kusisitiza uwajibikaji wa watendaji wa Serikali katika kutekeleza majukumu yao. Akifafanua hilo Rais Magufuli ametanabaisha kuwa nia kuu ya kubadilsha na kutengua baadhi ya watendaji wa Serikali ni kuhakikisha viongozi wanawajibika katika nafasi na majukumu yao.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimekuwa mstari wa mbele kuita uwajibikaji wa mamlaka na watendaji hasa pale wanaposhindwa kusimamia majukumu yao kisheria na wanaposhindwa kulinda na kudumisha haki za binadamu.

2. Usimamizi thabiti wa miradi ya maendeleo; kupitia hotuba yake Mhe. Rais amesisitiza matumizi sahihi ya fedha zinazotolewa na Serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za kijamii.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kuzingatia misingi ya haki ya maendeleo kwa mujibu wa *Tamko la Umoja wa Mataifa juu ya Haki ya Maendeleo 1986*, kinaunga mkono wito wa Rais kwa viongozi wa umma na mamlaka husika kuongeza umakini katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa lengo la kuongeza tija katika maisha ya watanzania wote.

3. Kubadilishwa kwa Sheria zisizo na manufaa kwa taifa; katika hotuba ya Mhe. Rais Magufuli ameweka wazi hamu yake ya kutaka kuona mabadiliko ya sheria zisizo na maslahi kwa nchi akitolea mfano Sheria ambazo zinazuia mfungwa aliyehukumiwa kunyongwa kufanya kazi za uzalishaji.


**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimekuwa mstari wa mbele kupinga Adhabu ya Kifo, kwani ni adhabu iliyo kinyume na haki za binadamu na isiyoinufaisha Serikali kwa namna yoyote ile. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza adhabu ya kifo kufutwa kabisa katika sheria za nchi.

4. Kuimarishwa kwa vyombo vya usalama nchini; akitoa maagizo kwa Waziri wa mambo ya Ndani, Rais Magufuli ameagiza kiimarishwa kwa utendaji na ufanisi wa vyombo vya usalama ikiwemo Jeshi la Zima Moto na Kikosi cha Usalama barabarani.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimependekeza mara kadhaa uimarishwaji wa vyombo vya usalama kimfumo na kiutendaji kwa lengo la kudumisha ulinzi wa haki za binadamu na utawala wa sheria.

5. Kukemea ubadhirifu na rushwa katika taasisi za Serikali; Mhe. Rais ameendelea kusisitiza mamlaka husika kuwachukulia hatua viongozi pamoja na taasisi za Serikali zinazoshiriki vitendo vya ubadhirifu wa mali za umma akitolea mfano ubadhirifu unaojitokeza katika baadhi ya manunuzi yanayofanywa na taasisi mbalimbali za umma.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapingana vikali na vitendo vya rushwa vinavyopelekea kuzorota kwa huduma za kijamii na hatimaye kupelekea maisha duni kwa wananchi. Tunaungana na Serikali kukekemea na kutaka hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya wabadhirifu.

6. Suala la Azaki za Kiraia; Mhe. Rais amekemea Asasi za Kiraia zinazojiendesha bila kuzingatia misingi ya sheria huku akisisitiza Asasi za Kiraia kufanyakazi kwa kufuata sheria za nchi. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua kuwa Asasi za Kiraia ziko kwa mujibu wa sheria na zinaendeshwa kwa kufuata Katiba ya nchi.

Mbali na hotuba ya Mhe. Rais kugubikwa na masuala ya msingi ya kitaifa yenye lengo la kustawisha nchi kiuchumi, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimebaini masuala kadhaa yanayopingana na misingi ya kidemokrasia. Baadhi ya masuala hayo ni kama ifuatavyo:

1. Kukosekana kwa uvumilivu wa kisiasa; katika hotuba yake Mhe. Rais ameonesha wazi kukerwa na maoni kinzani hasa yaliyotolewa na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kupinga *Mswaada wa Mabadiliko ya Sheria ya Tasnia ya Korosho ya mwaka 2009*. Hatua hii ni kinyume na misingi ya demokrasia ambayo inawataka wanasiasa kuzingatia hoja bila kujali misimamo na itikadi za vyama katika kufanya maamuzi yenye maslahi bora kwa wananchi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinasisitiza viongozi wa Serikali kufanya maamuzi kwa kuzingatia hoja zenye maslahi mapana kwa wananchi bila kujali misimamo na itikadi ya vyama.

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

2. Kuingiliwa kwa uhuru wa Bunge; katika hotuba yake Mhe. Rais ameonesha kutokuwa na imani na uendesheji wa shughuli za Bunge mathalani kwa kutamka wazi kwamba

hakuridhishwa na namna ambavyo mmoja ya wenyeviti wa Bunge alivyojaribu kuzuia hoja za moja ya Mbunge anayetetea Serikali. Kauli kama hiyo inadhorotesha misingi ya *Mgawanyo wa Madaraka* ambayo ni nguzo muhimu katika nchi inayoendeshwa kidemokrasia.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaikumbusha Serikali kutokuingilia utendaji wa mihimili mingine kinyume cha *Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.*

Mwisho, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapenda kuikumbusha Serikali ya Awamu ya Tano kuona haja ya kurejesha mchakato wa upatikanaji wa *Katiba Mpya* kwa lengo la kuweka mifumo imara ya uongozi na usimamiaji wa rasilimali za nchi.

**Imetolewa leo tarehe 03/07/2018 na,**

**Wakili Anna Henga**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**

**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member